# Learning by Ear 2010 – Urban Exodus

## Episode 07: "Failing the corrupt way"

**Author: Alfred Dogbé**
**Editor: Yann Durand**
**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI WA MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI WA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI WA 24, MWANAUCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- **NANA** (UMRI WA MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)

Onyesho la 2:

- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI WA MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN)
- **HADARI** (UMRI MIAKA 48, MKUU IDARA YA HUDUMA ZA MASHAMBANI)

Onyesho la 3:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI WA MIAKA 29)
- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- **NANA** (UMRI WA MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)

**Intro:**

Karibu kwenye *Learning by Ear* upate kipindi kipya miongoni mwa mfululizo wetu mpya wa "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko" kuhusu uhamiaji mijini. Baada ya kukata tamaa kwa jinsi mambo yalivyo mjini, Ben, Baki na Zeina, vijana watatu wasio na ajira na walio na shahada za chuo kikuu, wameamua kuanzisha chama cha ushirika kijijini kwao.

Wanataka kuimarisha mavuno mashambani. Mkutano mkuu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na wakulima wamehamasika sana kushughulikia mradi huo.

Leo, katika kipindi hiki cha saba, tutashuhudia jinsi chama kinavyotatizika kutokana na taratibu na kanuni zilizowekwa. Kundi zima liko nyumbani kwa Ben.

**Scene 1: At Ben's.**

**KABO, BEN, ZEINA, BAKI AND NANA.**

**1. ATMO: CRICKETS, HENS, SOUND OF POUNDING IN THE DISTANCE**

**2. SFX: INSTRUMENTAL MUSIC, LOW VOLUME, FROM THE RADIO**

**3. BEN** Mambo yanakwenda vizuri! Tumepewa shamba ili tuweze kufanya majaribio na kuwafunza wakulima mbinu ambazo nimekuwa nikizishughulikia. Ziada ya hilo, taasisi fulani ya utafiti wa kilimo imekubali kutupatia mbegu bora za jamii ya kunde pamoja na miti kuzuia mmomonyoko wa udongo ili kuongeza mazao. Mwasemaje?

| | | |
|---|---|---|
| **4.** | **BAKI** | Sawa hivyo Ben, lakini taasisi ya utafiti itatupatia mbegu hizi kwa masharti mawili: Ni lazima jambo hilo liidhinishwe na wakuu wanaohusika na inatubidi kugharamia uchukuzi wa mbegu hizo! |
| **5.** | **BEN** | Analosema Baki ni kweli. Nimekuwa kila mara nikienda ofisini kwa Hadari naye amekuwa akiniambia ataidhinisha kesho, wala kesho yenyewe haijafika. Kuna mara aliniambia niandike upya kumbukumbu za mkutano mkuu eti kwasababu hazikuwa zimefuata vigezo vinavyotakikana. Jana kanambia gari lake halina mafuta ya kufika kwenye makao makuu. |
| **6.** | **NANA** | Anataka kukutapeli! |
| **7.** | **BEN** | Basi atakula huu, Nana. Ninakuhakikishia hilo! |
| **8.** | **KABO** | Ndiyo, lakini huenda akazidi kutuchelewesha. |
| **9.** | **BAKI** | Ben, nipe hizo nyaraka. Ataziidhinisha lau sivyo nimzabe makonde! |
| **10.** | **ZEINA** | Huna ujualo ila fujo! |
| **11.** | **BAKI** | Zeina, huyo bwana analipwa mshahara kufanya hivyo, au siyo? Anapaswa kufanya kazi aliyoajiriwa kufanya! |
| **12.** | **BEN** | Bila shaka anapaswa kufanya hivyo! Bila shaka. Lakini twendeni taratibu. Acheni niende nimuone mwanzo. |
| **13.** | **BAKI** | Hatutampa japo senti moja ng'o! |

| | | |
|---|---|---|
| **14.** | **ZEINA, NANA & BEN** (**at the same time**) Hatutampa! | |
| **15.** | **KABO** | Sasa tuamue kufanya nini? Hawa watumishi wa umma wana ushawishi mkubwa. Wanaweza kukuharibia jambo lako kwa kujifanya kwamba wamesahau mpaka pale utakapokubali matakwa yao. |
| **16.** | **BEN** | Mambo yatabadilika! Ikishindikana nitakwenda makao makuu mimi mwenyewe! |
| **17.** | **KABO** | **(amused)** Loo! Ben unachekesha. Huko utapatana na wengine walafi na walaghai kumzidi Hadari. |
| **18.** | **BAKI** | Nasi tukikubali matakwa yao, hawataacha tabia hii mbovu. Ben anambembeleza Hadari. Ngoja nikaonane naye. |
| **19.** | **KABO** | Sawa, lakini nitaandamana nawe. |
| **20.** | **NANA** | Si hilo tu. Nadhani pia watu wanaendelea kupungukiwa na hamasa. Kina mama hawaji tena mikutanoni. Idadi ya kina mama 40 waliohudhuria siku ya kwanza imeshuka na kufikia kina mama kumi na wawili. Sijui kwa nini. |
| **21.** | **BAKI** | Na sijapata japo wanachama kumi kwa kipindi cha kwanza cha mafunzo. |
| **22.** | **BEN** | Tulipowaelezea juu ya huu mradi, wote waliuchangamkia! |
| **23.** | **BAKI** | Pengine tulikosea mbinu tuliyotumia kuwatangazia azma yetu. |
| **24.** | **NANA** | Mbinu gani hiyo? |

| | | |
|---|---|---|
| **25.** | **BAKI** | Nadhani kuna mtu anayedhamiria kuuvuruga mradi wetu! |
| **26.** | **NANA** | Tusilaumu watu wengine kwa matatizo yetu. |
| **27.** | **BEN** | Mimi mwenyewe nasema hivyo! |
| **28.** | **KABO** | Nana, Ben, pengine mnayosema ni kweli, lakini kama mjuavyo… Dalili ya mvua ni mawingu. Inatubidi kuzingatia sana yale watu wanayoyasema kuhusu chama chetu. |
| **29.** | **BAKI** | Wanakijiji wengi wanasema kwamba sisi ni maskini hata hatuwezi kusimamia shughuli zetu wenyewe. |
| **30.** | **BEN** | Ambalo ni kweli. |
| **31.** | **BAKI** | Ndiyo… lakini hilo lina maana kwamba hawatarajii kupata chochote kutoka kwetu. |
| **32.** | **NANA** | Kina mama wanasema kwamba tunaota. |
| **33.** | **BEN** | Wala tusife moyo. Watu hawana matumaini yoyote ya kufanikiwa maishani. Nadhani juhudi zetu na ari tuliyo nayo italeta mavuno na pia kuwapa matumaini. |
| **34.** | **ZEINA** | Lakini mradi wetu unahitaji matokeo ya moja kwa moja. |
| **35.** | **NANA** | Tingo huwapatia fedha ili wakuze njugu. |
| **36.** | **KABO** | Ndiposa inatubidi kukifanyia kazi chama chetu kiwe mfano wa kuigwa. |

**37. BAKI** Kabo, Twende tukazungumze na Hadari. Yuko afisini kwake sasa hivi.

**38. BEN** Nendeni! Mimi, Nana na Zeina tutabaki hapa tukizungumzia suala la mawasiliano na jinsi ya kupata rasilimali.

**39. SFX: STEPS (TWO PEOPLE) WALKING AWAY**

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: Hadari's office.**

**BAKI, HADARI AND KABO.**

**40. ATMO: OFFICE SOUNDS. COMPUTER KEYBOARD; TELEPHONE RINGING**

**41. HADARI** Sijamaliza kuzifanyia kazi nyaraka zenu. Njooni baada ya siku mbili!

**42. KABO** Lakini Bwana Hadari, jana ulituahidi kwamba utakuwa umekamilisha kazi hiyo hivi leo.

**43. HADARI** Kweli niliahidi. Samahani… Lakini jambo lenyewe gumu!

**44. BAKI** Kuna tatizo lolote? Kwani kuna jambo tulilolisahau?

**45. HADARI** Nyaraka zenu hazina neno… lakini hali yenyewe inatatiza na kwa hivyo ninahitaji muda zaidi kuzifanyia kazi…

| | | |
|---|---|---|
| **46.** | **BAKI** | Bwana Hadari! Kabla ya kuwasilisha maombi yetu tulivipitia vifungu vya sheria vinavyohusika na vyama vya ushirika, na tukafahamu kila la kufahamu. |
| **47.** | **HADARI** | Kwa hivyo? |
| **48.** | **BAKI** | Unachopaswa kutuarifu ni ikiwa mradi wetu unalingana na sera ya kitaifa kuhusu kilimo. Kazi yako iliyobaki ni kutia sahihi kwenye nyaraka zinazohusika. |
| **49.** | **HADARI** | Na unafikiri nitaidhinisha mradi huo vivi hivi bila kuupitia? Ni jukumu langu kuhakikisha kwamba kila kitu ki sawa! |
| **50.** | **BAKI** | Sivyo. Huna uwezo wa kutoa vibali kuviruhusu vyama vya ushirika kuendesha shughuli. |
| **51.** | **HADARI** | Uliyosema ni kweli. Mkuu wa eneo ndiye hutoa kibali lakini yote hayo hutegemea maoni yangu mimi. |
| **52.** | **BAKI** | Usituone wajinga! |
| **53.** | **HADARI** | Kama wajua mambo yanavyofanywa, mbona usijifanyie mwenyewe basi? |
| **54.** | **BAKI** | Unalipwa mshahara kufanya hiyo kazi! |
| **55.** | **HADARI** | Ninajua sana. Lakini mimi si mtumwa. Kwani kuna nini? |
| **56.** | **BAKI** | Si bure hivyo unavyofanya. Nadhani unataraji tukuhonge ili ushughulikie mradi wetu! |
| **57.** | **HADARI** | Nimefanya kazi hapa kijijini sasa yapata miaka mine. Ndiyo mara ya kwanza napata hizo shutma za kudai hongo. |

| | | |
|---|---|---|
| **58.** | **BAKI** | Basi mbona hutaki kushughulikia nyaraka zetu? Kwa nini unataka kukitatiza chama chetu cha ushirika? |
| **59.** | **HADARI** | Kijana nenda taratibu! Hivyo sivyo ninavyofanya kazi! |
| **60.** | **BAKI** | Natumai sivyo maana hatutakupa hata senti moja kwa huduma ambayo ni bure na ambayo ni haki yetu kisheria katika nchi hii. |
| **61.** | **KABO** | Endapo nyaraka zetu zina matatizo, tueleze. Tutajitahidi kurekebisha. |
| **62.** | **HADARI** | Hazina shida hata kidogo! Kuweni na subira na mrudi kesho saa nane! |
| **63.** | **BAKI** | (**calm but determined**) Hatuendi kokote. |
| **64.** | **HADARI** | Hivyo ni vitisho? |
| **65.** | **BAKI** | Chukulia utakavyo. |
| **66.** | **KABO** | Jamani tuacheni ugomvi! |
| **67.** | **HADARI** | Taratibu, kijana. Wewe si mkuu wangu kazini wala huwezi kuniagiza kufanya mambo unavyotaka wewe. |
| **68.** | **BAKI** | Ninatetea haki zangu. |
| **69.** | **HADARI** | Haki zako? |
| **70.** | **BAKI** | Bila shaka! Ni jukumu lako kushughulikia barua yangu ya maombi. |
| **71.** | **HADARI** | Kwani wewe nani? |

**72. BAKI** Anayepata huduma ya umma. Na wewe ni mtumishi wa umma. Unalipwa kufanya kazi na si kushinda baa.

**73. HADARI** Usinitukane!

**74. KABO** Ebu tuacheni fujo jama!

**75. HADARI** Utanitambua mimi nani!

**76. BAKI** Ichukue fomu, uiidhinishe kisha uitie sahihi. Hivyo tu. Wala haichukui muda.

**77. KABO** Bwana Hadari...

**78. HADARI** Tokeni ofisini mwangu!

**79. KABO** Bwana Hadari!

**80. BAKI** Siondoki hapa bila nyaraka zangu!

**81. KABO** Baki!

**82. HADARI** Tokeni ama nitawaondoa kwa nguvu!

**83. BAKI** Jaribu uone!

**84. HADARI** Acha tuone!

**85. SFX: NOISE OF A STRUGGLE. A CHAIR FALLING. A SHIRT BEING RIPPED. A TABLE BEING PULLED TO AND FRO. HEAVY BREATHING.**

**86. KABO** Acheni! Hivi sivyo matatizo yanavyotatuliwa! Acha mara moja! Baki!

**87. HADARI** Tokeni! Tokeni!

**88. BAKI** Ebu tuone!

**89. KABO** Kwani mna kichaa?

**90. HADARI** Nimewaambia mtoke! Tokeni!

**91. KABO** Tafadhali!

**92. BAKI** Aaa!

**93. SFX: SOUND OF A BODY COLLAPSING ONTO A PIECE OF FURNITURE AND THEN ONTO THE GROUND**

**94. KABO** Umemfanya nini?

**95. HADARI** Sijamgusa hata! Ameanguka mwenyewe!

**96. BAKI** (**groaning with pain**.)

**97. KABO** Balaa! Balaaa!

**98. HADARI** Ni jambo kubwa? Kijana? Je unanisikia?

**99. BAKI** (**groaning with pain**.)

**100. KABO** Hali yake si nzuri. Tumshughulikie haraka iwezekanavyo!

**101. HADARI** Tumpeleke kwenye zahanati, haraka!

**102. SFX: SOUND OF TWO PEOPLE TRYING TO CARRY A BODY**

**Scene 3: A street.**

**BEN, ZEINA AND NANA.**

**103. ATMO: STREET NOISES. TRAFFIC, ENGINES, HORNS**

**104. SFX: SOUND OF RAPID STEPS (THREE PEOPLE)**

**105. NANA** (**completely out of breath**) Siwezi tena kukimbia…!

**106. BEN** (**out of breath**) Tupumue kidogo. Zeina!

**107. ZEINA** Nataka nimwone!

**108. BEN** Zeina, tungoje!

**109. NANA** Hawezi kutusubiri.

**110. BEN** Tujitahidi kumfikia!

**111. SFX: RAPID STEPS**

**112. ZEINA** Nataka nimwone. Inanibidi nimwone Baki!

**113. NANA** Utamuona!

**114. BEN** Tuko karibu kufika!

**115. ZEINA** Je yu hai?

**116. BEN** Tumeshafika!

**117. ZEINA** Niambieni! Je yuko hai?

**118. BEN** Walisema hali yake si mbaya sana.

**119. ZEINA** Aliangukia kichwa. Hakuwa akifurukuta walipompeleka kwenye zahanati.

**120. BEN** Walitwambia kwamba alikuwa amepoteza fahamu!

**121. NANA** Daktari ni mzuri sana.

**122. ZEINA** Zahanati yenyewe haina vifaa. Watatumia nini kumtibu?

**123. NANA** Atapona kweli?

**124. ZEINA** (**bursting into tears**) Oh… oh… lolote litakalomfika…

**125. NANA** Hakuna litakalomfika.

**126. ZEINA** (**still crying**) Ni kosa langu! Ni kosa langu!

**127. BEN** Acha huo upuuzi!

**128. BEN** Twendeni!

**129. ZEINA** Hakutaka kuja huku kijijini. Alinuia jambo moja – kwenda zake Marekani. Mimi ndiye niliyemshurutisha kuja huku. Nilijua alifanya hivyo kwa kuwa ananipenda. Na sasa…

**130. NANA** (**in tears**) Zeina kwa hisani yako! Usiseme hivyo!

**131. BEN** Acheni kulia. Watu watashangaa halafu wataanza kutufuata. Twendeni. Ninaamini tayari ameshazinduka, na hali yake ni sawa. Twendeni tukamuone!

**132. ATMO: SNIFFING AND CRYING CONTINUE.**

**133. SFX: STEPS GOING AWAY.**

**Outro:**

Na huo ndio mwisho wa kipindi cha saba cha vipindi vyetu vya Learning by Ear kuhusu uhamiaji mjini viitwavyo "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko".

Usikose kipindi kijacho ili ujue hatima ya Bari hospitalini baada yake kugombana na Hadari.

Kama unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuandikia maoni fungua ukurasa wetu wa tovuti dw-world.de/LBE au utuandikie barua-pepe kupitia anwani yetu lbe@dw-world.de.

Kumbuka kutusikiliza tena kipindi kitakachofuata!

**END OF EPISODE 7**